

TANGAZO

la

CHANIKIWITI



na

HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD

Masibi Mau'udi na Imam Mahdi^{as}

TĀNGAZO LĀ CHĀNIKIWĪTI

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} wa Qadian
Masihi Mau‘udi na Imam Mahdi

TANGAZO LA CHANIKIWITI
Tafsiri ya Kiswahili ya: *Sabz Ishtihar* (Urdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} wa Qadian

Mfasiri: Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1888
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2019

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-84880-532-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ
نَحْمَدُهُ وَنُصَلِّي عَلَى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ

MAELEZO YA MWENEZI

KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyahidiwa na Imam Mahdi a.s. alizaliwa tarehe 13 February 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alikubali kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo alielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi ya maana sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi

inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam Mahdi na Masihi Aliyahidiwa, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume saw. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha nidhamu ya Ukhilifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a

KUHUSU KITABU

Hadhrat Masihi Aliyahidiwa a.s. alitoa bishara moja, tarehe 20 Februari 1886 kuhusu kuzaliwa kwa mwana mtukufu. Bishara hiyo inajulikana kuwa *Bishara kumhusu mwana aliyahidiwa*. Wakati Bashir wa kwanza, mwana wa Seyyidna Ahmad as. alipofariki katika umri mdogo tarehe 4 Novemba 1888 ndipo wapinzani walipiga makelele kwamba mwana aliyahidiwa amefariki haraka sana badala ya kupata umri mrefu sawa na utabiri. Seyyidna Ahmad a.s.

kwa kuondoa mashaka yao na kujibu upinzani wa wapinzani aliandika kijitabu hiki katika mwaka 1888 na akathibitisha kwamba Bashir wa kwanza hakuwa mwana aliyeahidiwa bali sawa na ahadi ya Mwenyezi Mungu mwana aliyeahidiwa lazima atazaliwa katika muda wa miaka 9. Jina lenyewe la kijitabu hiki ni '*Hotuba ya kueleza Uhakika alipofariki Bashir*', lakini kwa sababu karatasi zilizotumiwa kwa kuchapa kijitabu hiki zilikuwa za rangi ya chanikiwiti, kilitambulika kwa jina la 'Tangazo la Chanikiwiti'.

SHUKURANI

Kijitabu hicho kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta wa Tanzania. Kisha hapa Makao Makuu katika 'Deski ya Kiswahili' ya wakalati Tasnif Rabwah, Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani na Sheikh Mubarak Mahmood wakaichunguza tafsiri hiyo kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana na kuidurusu. Aidha ndugu kadha wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal na Sharifu Tanvir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu

Awajaalie malipo bora na akubali huduma yao.
Aamina

Chaudhry Muhammad Ali, M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid,
Rabwah, Pakistan.
20th October, 2010

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ¹

الْحَمْدُ لِلَّهِ وَالسَّلَامُ عَلَى عَبَادِهِ الَّذِينَ اصْطَفَى²

HOTUBA YA KUELEZA UHAKIKA ALIPOFARIKI BASHIR

Iwe wazi kuwa kutokana na kifo cha mwanangu Bashir Ahmad, ambaye alizaliwa mnamo tarehe 7 Agosti mwaka 1887, siku ya Jumapili, na aliitwa kwa Mwabudiwa wake wa kweli mnamo tarehe 4 Novemba mwaka 1888, katika siku hiyo hiyo ya Jumapili, akiwa katika umri wake wa miezi kumi na sita, majira ya sala ya Alfajiri, kelele za ajabu ziliibuka toka kwa watu wenyewe fikara isiyopevuka na jamaa wakasema maneno ya namna namna, na zikatolewa rai mbali mbali za kijinga zilizotoka katika nyoyo zilizopindamana. Wapinzani wa dini ambao tabia yao ni kufanya hiyana na uzushi katika kila jambo, wakaanza kukizulia aina mbali mbali za uzushi kifo cha mtoto huyu. Hivyo, ingawa

¹ Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

² Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, na amani iwe juu ya watumishi wake wateule.

mwanzoni hatukuwa na dhamira ya kuchapisha tangazo au hotuba yoyote juu ya kifo cha mtoto huyu maasum, wala hakukuwa na haja ya kuchapisha, kwa sababu kulikuwa hamna jambo lolote humo ambalo lingeweza kuwa sababu ya kutetereka kwa mtu mwenye fahamu zake. Lakini kelele hizi zilipofikia kileleni na ikaonekana kuwa athari zake zenye madhara zinafika hata kwenye nyoyo za Waislamu dhaifu wasio na upeo wa ufahamu, ndipo tukaona inafaa kuchapisha hotuba hii kwa ajili tu ya Mungu. Sasa iwe wazi kwa wasomaji kuwa baadhi ya wapinzani wameandika kwa kejeli ndani ya vipeperushi na magazeti yao kuwa eti huyu ndiye yule mtoto ambaye kuhusuye ilielezwa katika tangazo la tarehe 20 Februari 1886, na 8 Aprili 1886 na 7 Agosti 1887 kwamba atakuwa ni mwenye heshima, taadhima na mali, na mataifa yatapata baraka toka kwake. Na baadhi yao wakitunga wenyewe uzushi³

³ Mzushi huyu ni Lekhram wa Peshawar ambaye ametaja matangazo yote hayo matatu yaliyotajwa hapo juu katika matini kwa lengo la kuthibitisha madai yake, na akafanya hiyana tupu. Kwa mfano akitaja tangazo lile la 8 Aprili 1886 ameandika ibara ya tangazo hilo ndani ya kipeperushi chake kwamba: "Nikabainikiwa kiasi hiki kwamba ni karibuni sana mwana atazaliwa katika kipindi ambacho hakiwezi kuzidi muda wa himila moja", lakini sentensi inayofiuatia ibara hii, yaani sentensi hii kwamba: "Hii haikudhihirishwa kuwa

wakaandika pia ndani ya tangazo lao kwamba kuhusiana na mtoto huyu ufunuo huu pia ulielezwa kuwa atawaoa mabinti wa wafalme. Lakini ibainike kwa wasomaji kuwa wale watu waliota shutuma hii wamedanganyika mno au wametaka kudanganya. Ukweli hasa ni huu kuwa hadi mwezi wa Agosti 1887, ulio mwezi wa kufariki⁴ kwa mtoto aliyefariki, matangazo yote niliyoyachapisha ambayo Lekhram

mwana atakayezaliwa sasa ndiye yule yule au atazaliwa wakati mwingine katika muda wa miaka tisa." Sentensi hii hakuiandika kusudi, kwa sababu haikumfaa kusudio lake na ilikuwa yenye kuukata mzizi wa fikara yake mbovu. Halafu, hiyana ya pili ni kwamba kabla ya kipeperushi hiki cha Lekhram kulishachapishwa kipeperushi kingine na Waarya katika kiwanda cha uchapishaji cha Chashmae Nur cha huko Amritsar, ili kujibu matangazo yetu hayo matatu yaliyotajwa hapo juu; humo wamekiri kwa uwazi kabisa kwamba kwa kuzingatia matangazo yote hayo matatu haithibitiki kuwa mwana aliyezaliwa ndiye yule Msuluhishi Aliyahidiwa na mwenye kupata umri mrefu au atakuwa mwingine. Lekhram hakukiri habari hiyo popote pale. Ni dhahiri, basi, kwamba kipeperushi cha awali cha Waariya chenyewe cha king'olea mbali kipeperushi hiki cha Lekhram. Tazameni kipeperushi chao hicho ambaco kichwa chake cha habari sawa na hali yao ni hii

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمَاْكِرِينَ

Mwenyezi Mungu Hawapendi wafanyao hila.

Mwandishi.

⁴ Hii ni kosa la mwandikaji, badala ya "kufariki" sahihi ni "kuzaliwa." (Mwenezi)

wa Peshawar ameyarejea katika kipeperushi chake kama ushahidi wa madai yake, hakuna mtu ye yote awezaye kuonyesha humo herufi hata moja ambamo mmedaiwa kuwa huyu huyu mtoto aliyefariki ndiye Musilim Mau‘udi na mwenye kupata umri mrefu. Bali tangazo la tarehe 8 Aprili 1886 na pia tangazo la tarehe 7 Agosti 1887 ambalo kwa sababu ya marejeo ya tangazo la tarehe 8 Aprili 1886, lilichapishwa siku ya kuzaliwa Bashir, linaeleza kwa uwazi kwamba kwa ufunuo bado haijamuliwa kuwa je huyu mwana ndiye Msuluhishi Aliyahidiwa na mwenye kupata umri mrefu au kuna mwingine? Ni ajabu kwamba Lekhram wa Peshawar akishikwa na jadhba ya uadui alileta ukinzani, kwa kuyataja matangazo hayo, katika kipeperushi chake hicho kilichojaa matusi na lugha chafu, ilivyo tabia yake ya asili, lakini hakuyasoma matangazo hayo matatu akiwa ameyafumbua macho, ili angeepuka majuto ya papara. Ni sikitiko kubwa, kwa nini Mapanditi wa Kiarya hawawakatazi wazushi hawa kuongopa ambao wakisimama mitaani wayaeleza mafundisho yao kwamba kuacha na kuepuka uwongo na kuuamini ukweli na kuukubali ni imani ya Waarya. Ni jambo la ajabu, basi, kwamba imani hii daima hudhihirishwa kwa kauli tu lakini kwa wakati wa vitendo huwa haifai hata mara moja. Ole wao mara elfu!

Basi, mazungumzo kwa kifupi ni kwamba matangazo yote haya mawili yaliyotajwa hapo juu, ya tarehe 8 Aprili 1886 na 7 Agosti 1887, hayaelezi asilani kwamba mtoto azaliwaye ni wa namna gani na mwenye sifa zifi, bali matangazo hayo mawili yanatoa ushahidi wa uwazi kwamba jambo hili, kulingana na ufunuo, bado halijatolewa maelezo wala halijafafanuliwa.⁵ Naam, sifa hizo zilizoelezwa hapo juu kuhusiana na mwana aliyetabiriwa kuja, kwa kwaida zimeelezwa kabisa ndani ya tangazo la tarehe 20 Februari 1886 bila kumtaja yejote wala kumwainisha. Lakini hakuna popote ndani ya tangazo

⁵ Ibara ya tangazo la tarehe 8 Aprili 1886 ni hii: Karibuni sana atazaliwa mwana ambaye hawezi kupitisha muda wa mimba moja. Lakini hii haikudhihirishwa kwamba huyo atakayezaliwa sasa ndiye huyo huyo mtoto au atazaliwa katika wakati mwingine ndani ya muda wa miaka tisa. Tazameni tangazo la tarehe 8 Aprili 1886 lililochapishwa na kiwanda cha uchapishaji cha ‘Chashmae Faiz Qadirii, cha Batala. Ibara ya tangazo la tarehe 7 Agosti 1887 ni hii: Enyi wasomaji! ninakupeni habari njema ya kwamba yule mtoto ambaye kuzaliwa kwake nilitoa bishara ndani ya tangazo la tarehe 8 Aprili 1886, yeye amezaliwa mnamo tarehe 16 Dhilkaadi sawa na tarehe 7 Agosti. Tazameni tangazo hayo matatu ambayo Lekhram wa Peshawar ameyatoa kwa hamaki, inapatikana hata ishara ya jambo hili kwamba wakati wowote tulimueleza mtoto huyu aliyefariki kuwa ndiye Msuluhishi Aliyahidiwa na atakayekuwa na umri mrefu? Basi tafakarini na zingatieni.

hilo mlimoandikwa kwamba mtoto atakayezaliwa tarehe 7 Agosti 1887 ndiye huyo huyo atakayekuwa na sifa hizo, bali katika tangazo hilo hamna tarehe yoyote iliyotajwa ya kuzaliwa kwa mtoto huyo kwamba atazaliwa lini na wakati gani. Hivyo, kudhania kwamba ndani ya matangazo hayo mwana huyu aliyefariki ndiye aliyesemwa kuwa na sifa hizo, ni ukaidi na udanganyifu kabisa. Matangazo hayo yote tunayo, na wasomaji wengi watakuwa nayo. Inafaa myasome kwa makini halafu wenyewe mfanye uadilifu. Huyu mtoto aliyefariki alipozaliwa, basi baada ya kuzaliwa kwake nilipata mamia ya barua toka sehemu mbali mbali kwa kuuliza kwamba je, huyo ndiye yule yule Msuluhishi Aliyahidiwa ambaye kwa njia yake watu watapata mwongozo. Wote hao waliandikiwa jibu hili hili kwamba hadi sasa sijafunuliwa ufunuo wowote wa wazi kuhusiana na jambo hilo. Naam, kwa njia ya Ijtihadi ilidhaniwa kwamba si ajabu kama huyo huyo mtoto awe ndiye Msuluhishi Aliyahidiwa. Na sababu yake ilikuwa ni hii kwamba sifa nyingi za huyu mtoto aliyefariki zilikuwa zimeelezwa katika funuo ambazo zilikuwa zinahusiana na roho yake iliyotakata na asili yake iliyotukuka na nguvu zake za hali ya juu na kipaji chake king'aacho na wema wake wa kiasili, na zilikuwa na uhusiano na vipawa vyake vilivyokamilika. Basi, kwa kuwa zile adhama zilizokuwamo nafsini mwake hazikuwa na ulazima wa kupata umri mrefu, hivyo rai hii haikudhihirishwa

kwa yakini, kwa msingi wa ufunuo wowote kwamba huyu mtoto lazima atapata umri mpevu. Na kutokana na wazo hili na kusubiri huku uchapishwaji wa *Siraaje Muniir* ukasitishwa ili uhakika wa mwana huyu utakapofunguka wazi kabisa kwa njia ya ufunuo, ndipo hali yake iandikwe kwa mapana na marefu. Basi ni ajabu, tena ajabu sana kwamba ijapokuwa tulikaa kimya kabisa hadi sasa tusieleze rai yoyote kiufunuo kumhusu marehemu mwanangu wala hatukuchapisha ufuno wowote ule kuhusu habari hii, basi ni nani aliyepuliza ndani ya masikio ya wapinzani wetu kuwa eti sisi tumeshachapisha tangazo la aina hiyo.

Ikumbukwe pia kuwa ikiwa sisi kwa msingi wa dhana hii kwamba adhama za dhati za mwana marehemu zimejulikana kwa njia ya ufunuo, na akapewa jina Mubashir na Bashir na Nuruallah Swayyib na Charagh Din na majina mengineyo yaelezayo ukamilifu wake wa dhati na mwanga wake wa asili, hata kama tungechapisha tangazo lenye maelezo kwa mapana na marefu na humo, kwa kutaja majina hayo, tungeandika rai yetu hii kwamba labda Msuluhishi Aliyahidiwa na mwenye kupata umri mrefu atakuwa huyu huyu mtoto, hata hivyo machoni mwa wenyewe busara maelezo yetu haya ya kijitihadi yasingekuwa wenyewe kustahili lawama. Kwani mawazo yao maadilifu na mtazamo wao wenyewe maarifa ungewafahamisha mara moja kuwa kijitihadi hii

imefanywa kwa kuangalia yale majina tu machache ambayo yenyewe hayajawa wazi bali ni yenyewe maana mbalimbali tofauti na yanahitaji ufumbuzi. Hivyo, katika fikara yao hata kama hili lingekuwa ni kosa la kijitihadi, hata hivyo wangeliona ni la daraja la chini tu na la uzito mdogo na hafifu kabisa. Kwani ingawaje ni vigumu mno kumfahamisha mzito wa akili na mwenye moyo uliopofuka kanuni ile ya asili ya Mwenyezi Mungu ambayo tangu zamani sana inahusiana na wahyi, ruya, kashfi na funuo vilvyo na maana zaidi ya moja, lakini watu wenyewe utambuzi na busara wanafahamu wenyewe kuwa katika mambo ya bishara n.k., hata kama mtu akikosea kuelewa muradi wake hasa, basi hiyo haiwezi kuwa yenyewe kustahili kulaumiwa, kwani manabii wengi na mitume walio imara pia walipata kukosea kidogo katika kuainisha maana hasa ya Kashfi na Bishara zao zilizojifumba.⁶

⁶ Inadhihirika kutokana na baadhi ya ibara za Taurati kuwa Hadhrat Musa a.s. alipata kufanya makosa katika kufahamu na kufahamisha baadhi ya bishara zake, na yale matumaini waliyopewa wana wa Israeli ya kukombolewa haraka sana bila kukawia hayakutimia hivyo. Kwa hiyo wana wa Israeli wakiona hali iliyoko kinyume na matumaini hayo na kunyong'onyea nyoyoni, wakati mmoja, kwa kuchoka na hali wakapata kusema kwa sababu ya ufinyu wa mawazo yao uliokuwemo ndani ya silika yao kwamba, 'Ewe Musa na Harun! Mungu Akutendeeni kama mlivyotutendea.' Inaonekana kwamba kuchoka huku kwa kaumuhii yenyewe mawazo finyu kulitokea kwa sababu walivyoamini moyoni mwao kupata kuokolewa haraka sawa

Na wafuasi wao wenyewe mioyo izindukayo na dhamiri zing'aazo hawakustajabia katu wala hawakuhangaika kwa makosa hayo, kwa sababu walikuwa wakifahamu kuwa makosa hayo hayakuwemo kwenye funuo wala kashfi zenyewe, bali makosa yalifanyika katika kutoa maelezo. Basi ni dhahiri kwamba kama kosa la

na maelezo ya Musa haikutokea hivyo na hapo katikati matatizo yalitokea ambayo wana wa Israeli hawakupashwa habari zake kwa uwazi hapo kabla. Sababu yake ilikuwa hii tu kwamba hata Hadhrat Musa a.s. pia mwanzoni mwa matatizo yaliyotokea katikati na kurefuka kwayo hakupashwa habari wazi wazi; hivyo mwelekeo wa mawazo yake, kwa njia ya ijtihadi, ukawa umeelekeea kiasi fulani upande huu kwamba kutokana na ishara zile zilizo wazi Firauni asiye na auni atahiliki kwa haraka sana. Hivyo Mwenyezi Mungu, sawa na suna Yake inayoendelea kwa manabii wote tangu azali, kwa ajili ya kumjaribu Hadhrat Musa a.s. katika siku za mwanzo na kwa nia ya kumtilia hofu kwamba Hamhitaji yejote, Akamficha baadhi ya matatizo ya katikati, kwani kama tangu mwanzo angefunuliwa wazi wazi mambo yote yajayo na matatizo na shida zote Zitakazotokea, basi moyo wake ungepata nguvu na utulivu kamili, hapo hofu ya majoribio hayo ingeondoka moyoni mwake ambayo ilikwishapangwa katika utashi wa Mungu kumletea Hadhrat Musa na wafuasi wake kwa lengo la kuwapandisha madaraja na kuwapatia thawabu katika Akhera. Vivyo hivyo, yale matumaini na habari njema ambazo Yesu aliwapa wanafunzi wake ndani ya Injili kuhusiana na maisha ya dunia hii na mafanikio na hali njema nazo zilikuwa zikionekana zitapatikana kwa njia rahisi mno na kwa haraka sana. Na kutokana na maneno ya kibishara aliyyoyatoa Hadhrat Masihi a.s. hapo mwanzoni, ilikuwa inaonekana kana

kiijtihadi la wanazuoni wa elimu ya dhahiri na wa ndani haliwezi kuwa sababu ya wao kupungukiwa shani yao — nasi hatujafanya kosa lolote lile la kiijtihadi pia ambalo tungechapisha kwa uwazi na yakini kabisa katika tangazo lo lote — kwa nini, basi, wapinzani wetu wasio na busara wamepiga kelele

kwamba wangeupata ufalme madhubuti katika zama hizo hizo. Kutokana na dhana ya ufalme huo huo wanafunzi wake wakanunua hata silaha kwamba zitawafaa watakapotawala. Halikadhalika kuteremka kwake Hadhrat Isa a.s. mara ya pili bwana huyo msifika alieleza kwa midomo yake mwenyewe kwa maneno ambayo hata wanafunzi wake wakafahamu kwamba kabla hawajafa watu wa zama hizo wala wanafunzi wake hawajanywa kikombe cha mauti Hadhrat Masihi atakuwa amekuja tena duniani kwa ujalali na taadhima. Na inaonekana kwamba mawazo na rai ya Hadhrat Isa a.s. ilikuwa imeelemea zaidi kwenye fikara ile ile aliyotilia moyoni mwa wanafunzi wake ambayo kwa hakika haikuwa sahihi, yaani humo mlikuwemo na kosa kiasi fulani la kiijtihadi. Na ajabu zaidi ni hii kwamba imeandikwa pia ndani ya Biblia kuwa wakati fulani Manabii mia nne wa wana wa Israeli walitoa habari kuhusiana na ushindi wa mfalme fulani lakini haikutimia; yaani badala ya kushinda, kashindwa. Tazameni 1 Wafalme 22:19. Lakini katika bishara yangu yoyote ile hakuna kosa lolote la kiufunuo. Ufunuo ulidhihirisha kabla ya kutokea, kuzaliwa kwa wana wawili na kubainisha kuwa baadhi ya wana watafariki katika umri mdogo. Tazameni tangazo la tarehe 20 Februari 1886 na tangazo la tarehe 10 Julai 1888. Hivyo, kulingana njia bishara ya kwanza mwana mmoja akazaliwa na akafariki. Na mwana wa pili ambaye ufunuo ulieleza kumhusu yeye kuwa; utapewa Bashir wa pili ambaye jina lake la pili

kiasi hiki alipofariki Bashir Ahmad? Je, wanao ushahidi wa kutosha na wa kisheria, wa maandishi hayo au bila ya haki wanawadhihirishia watu mara kwa mara maono ya nafsi zao zinazowaamirisha kutenda maovu? Na hapa nastaajabia pia hali ya baadhi ya Waislamu wajinga kwamba kwa kuwaza nini wanatiliwa wasiwasi mwingi. Je, wanalo tangazo letu lolote lile linalowapa yakini kwamba sisi tulishakata uamuzi kwa ufunuo kwamba huyu ndiye yule yule mwenye kupata umri mrefu na Muslih Mau‘udi? Kama lipo tangazo lolote la aina hii, kwa nini halitolewi? Tunawahakikishia kwamba sisi hatujachapisha tangazo lolote la aina hiyo. Naam, Mwenyezi Mungu Alitudhihirishia katika baadhi ya funuo kuwa huyu mtoto aliyefariki alikuwa na vipawa vya hali ya juu, na jadhba za kidunia ziliondelewa mbali kabisa katika tabia yake na mmejaa ndani yake mng’ao wa kidini, naye ndiye mwenye asili yenye nuru na sifa za hali ya juu na roho ya kisiddiki, na anayo majina kama 'Mvua ya Rehema' na Mubashir na Bashir na Mkono wa Mungu kwa ujalali na jamali

ni Mahmud, ingawa huyo hadi sasa, yaani tarehe 1 Desemba 1888, bado hajazaliwa, lakini sambamba na ahadi ya Mwenyezi Mungu lazima atazaliwa ndani ya muda aliowekewa. Ardhi na mbingu zaweza kutanguka, lakini haiwezekani ahadi Zake zitanguke. Mjinga anazicheka funuo Zake na mpumbavu anazifanyia dhihaka bishara Zake takatifu, kwani siku ya mwisho imefichama machoni mwake na hatimaye imefichika kwa macho yake. Mwandishi.

na majina mengineyo. Basi, sifa zake Alizodohihirisha Mwenyezi Mungu kwa funuo zake, hizo zote zilikuwa ni sifa zake zinazohusiana na vipawa vyake ambazo hazikuwa na ulazima wa kujitokeza kidhahiri. Dai langu lihakikishwalo na dalili na liingialo akilini ni kwamba watoto wa wanadamu wajao katika dunia hii na nguvu za aina mbalimbali, wakipata umri mkubwa au wakifariki utotonu, lazima hutofautiana katika vipawa vyao vya kiasili na huonekana tofauti ya wazi katika nguvu zao, tabia zao, sura zao na akili zao, kama vile katika shule pengine watu wengi wamewaona baadhi ya watoto ambaao ni wenye akili nzuri na ufahamu mkubwa, wenye busara na wenye kuzingatia upesi na huipata elimu kwa haraka kana kwamba wanaendelea kunja jamvi kwa haraka, lakini umri wao hukoma na wanafariki tu katika umri mdogo. Na wako wengine ambaao ni mabwege na mambubumbu na wana sehemu ndogo sana ya uanadamu na wanadondokwa na udenda mdomoni na kuonekana hawakustaaribika na wengi wao wanakufa wakiwa wazee na wakongwe, na kwa sababu ya kukosa sana kipaji cha kiasili wanaondoka kama walivyokuja. Ilmuradi, kila mtu anaweza kuuona kwa macho yake mfano wa jambo hili kwamba baadhi ya watoto wanaumbika kikamilifu kiasi hiki kwamba ndani ya asili yao wanao utakaso wa masiddiki, nguvu za kiakili za wanafalasfa na dhamiri yenye nuru ya wenye maarifa na wanaonekana kuwa watapata kukua vizuri, lakini hawaishi katika

ulimwengu huu usio wa kudumu. Na pengine watu wamewahi kuona kuna baadhi ya watoto ambao alama zao hazionekani kuwa nzuri, na busara inatoa hukumu kwamba kama wakipata umri mrefu basi watatokea kuwa habithi sana, wenyе shari, majahili na wasiotambua haki. Ibrahim, mtoto kipenzi cha Mtume s.a.w., ambaye alifariki utotoni, yaani katika umri wa miezi kumi na sita, sifa za vipawa vyake safi na sifa za asili yake ya kisiddiki zimethibitika ndani ya Hadithi. Halikadhalika yule mtoto aliyeuawa utotoni na Hadhrat Hidhri, hali ya uhabithi wa tabia yake ni dhahiri shahiri kutokana na maelezo ya Kurani Tukufu. Mafundisho ya Islam kuhusiana na watoto wa makafiri wanaokufa katika umri mdogo nayo kwa hakika ndiyo sawa na kanuni hii kwamba vipawa vyao ni vipungufu kwa sababu:

الْوَلُدُ سِرْلَانِي⁷

Ilmuradi, kwa sababu ya usafi wa vipawa vyake na mng'ao wa asili yake halisi na mnasaba wake kamili wa kidini, mwana aliyefariki aliiwtwa katika ufunuo majina hayo ambayo yametajwa sasa hivi. Sasa kama mtu akitumia nguvu, anataka kufanya juhud kuhakikisha kwamba majina hayo yanamaanisha umri mrefu, basi huo utakuwa ni ukorofi wake — jambo ambalo kuhusu hilo hatujawahi kudhihirisha kabisa

⁷ Yaani mtoto ni siri ya baba yake.

rai yoyote iliyo ya yakini na ya mwisho. Naam, ni kweli, tena kweli kabisa, kwamba kwa kufikiria zile fadhila zake kulikuwa kunafikiriwa kwamba huenda huyu mtoto ndiye yule Muslih Mau‘udi (Mwana Aliyeahidiwa), lakini hii ilikuwa ni dhana tu ambayo haikuchapwa kwa njia ya tangazo. Hali ya Mabaniani inastaajabisha sana kwamba juu ya kusikia maelfu ya habari toka kwenye vinywa vya wanajimu na wapiga ramli wao ambazo hatimaye hutokea moja kwa moja kuwa upuuzi, hazina maana na uongo, hata hivyo hawakomi kuwaamini na hutoa udhuru kuwa eti makosa yamefanyika katika mahesabu, waila hakuna shaka yoyote katika ukweli wa ramli. Tena juu ya itikadi hizo za kijinga na mbovu huzishambulia bishara za ufunuo kwa sababu ya uadui bila ya kupata kosa lolote la wazi na lilio dhahiri. Tena, haidhuru kama Mabanyani watoe maneno ya aina hii mdomoni mwao yasiyo na msingi, kwa sababu wao ni maadui wa dini na daima wanayo silaha moja tu dhidi ya Islam nayo ni uongo na uzushi, lakini jambo la kustaajabisha sana mno ni hali ya Waislamu ambao juu ya kudai kuwa ni watu wa dini na wenye utawa na juu ya kuwa na itikadi za Kiislamu, bado wanatoa maneno ya kipuuzi ya aina hiyo. Kama wangeliyaona matangazo yetu ambamo kwa kukisia tungelikuwa tumesema kuwa mtoto huyo aliyefariki ndiye Mwana Aliyeahidiwa na mwenye kupata umri mrefu, hata hivyo ufahamu wa imani yao na utambuzi wa maarifa yao ilitakiwa kuwaelewesha kuwa hiyo ilikuwa ni

kosa tu la kijtihadi ambalo wakati mwingine huwatokea hata wanazuoni wa elimu ya dhahiri na batini, bali hata manabii pia wenye imara hawakuepukana na hali hiyo. Lakini hapa halikuchapishwa katu tangazo lolote la aina hiyo. Wamefanya haraka sana sawa na mithali kwamba bado mto haujaonekana lakini wao wameshatoa viatu tayari. Na ikumbukwe kwamba mistari hii michache tulioiandika kuwalusu Waislamu wa kawaida, imeandikwa kwa kuwahurumia kweli ili waepukane na wasiwasi wao usiokuwa na msingi na wala wasipate mioyoni mwao itikadi mbovu na potovu ya aina hii ambayo haina asili yoyote iliyo sahihi. Kuingiwa na wasiwasi kutokana na kifo cha Bashir Ahmad kunadhihirisha ujinga wao na kutofahamu kwao waila hakukuwa na sababu ya hitilafu na kukosoa. Tumeshaandika mara kwa mara kwamba hatujatoa tangazo lo lote ambamo tumedhihirisha kwa kauli moja na yakini kwamba huyu huyu mtoto ndiye yule Muslih Mau‘udi na atakayepata umri mrefu. Na ingawa kwa njia ya ijtihadi, kutokana na alama zake za dhahiri, tulikuwa tumeelekea kiasi fulani kwenye wazo hilo, lakini kutokana na sababu hiyo hiyo wazo hilo halikuchapiswa kabisa katika matangazo, kwani bado hilo ni la kijtihadi, ili kama ijtihadi hii haikutokea kuwa sahihi, basi watu wa kawaida ambao hawana habari na maarifa ya ndani ya elimu ya Kiungu wasije kudanganyika. Lakini yasikitisha mno kwamba watu wa kawaida walio kama wanyama

hawakuepuka kudanganyika na wakatoa maelezo mabovu walivyotaka. Hawafikirii kabisa kwamba msingi wa upinzani wao ni dhana hii tu kwamba kwa nini kosa la kijtihadi lilitokea. Sisi twatoa jibu lake kwamba hakuna kosa lolote la kijtihadi lilitokea kwetu ambalo kwa neno zima na kwa yakini na kulitegemea tukalichapisha kwa jumla. Haya, tukilegea kidogo twauliza kwamba kama Nabii ye yote au Walii akiwahi kufanya kosa katika kukadiria na kuainisha bishara fulani yamhusu nani, je kosa la aina hii laweza kumpunguzia au kumkasiria chochote katika daraja lake la unabii au uwali? Hapana kabisa! Mawazo yote haya hutokeea kwa sura ya upinzani kwa sababu ya ujinga na kutokuelewa. Kwa kuwa katika zama hizi ujinga umetapakaa sana na watu hawazijali kabisa elimu za kidini, ndiyo sababu hata jambo lililo sawa laonekana limepotoka. Waila jambo hili limeaminiwa na wote na kukubaliwa kwamba kila Nabii na Walii huweza kufanya kosa katika kukadiria na kuainisha kashfi na bishara zake zamhusu nani pale ambapo hakufafanuliwa vizuri na Mwenyezi Mungu, na kosa hilo haliwapunguzii hata kidogo shani ya hao Manabii na Wateule, kwani elimu ya Wahyi nayo ni elimu mojawapo mionganoni mwa elimu. Na ile kanuni ya maumbile na kanuni ya asili ihusikanayo na elimu na fani zote iingiliapo kati nguvu ya kutafakari, elimu hiyo haiwezi kuwa nje ya kanuni hiyo. Na wale watu mionganoni mwa Manabii na Mawali waliojaaliwa

elimu hii, huwa wanalazimika kuwa na mambo yote yahusikanayo na hiyo pia, yaani huwa yanawapata likiwemo pia kosa la ijtihadi. Basi, kama kosa la ijtihadi lastahili kulaumiwa, hapo Manabii na Mawalii na wanazuoni wote wanashirikiana katika lawama hii.

Msifikirie kuwa kutokana na kosa lolote la kijtihadi inapungua shani na adhama ya bishara hizo zitokazo kwa Mungu au zinakuwa hazina manufaa sana kwa wanadamu au huleta hasara kwa dini na kwa kundi la wanadini, kwa sababu hata kama kuwe na kosa la kijtihadi, hilo hutokea tu kwa muda kama jaribio, halafu nuru za ukweli hudhihirika kwa wingi sana mno na misaada ya Mungu huonyesha midhihirisho yake kana kwamba jua linachomoza na magomvi yote ya mahasimu yanásuluuhishwa kwayo. Lakini kabla ya kudhihiri mchana huo ung'ao ni lazima waliotumwa na Mwenyezi Mungu wapate kujaribiwa vikali, na wafuasi wao nao wachunguzwe barabara na kutahiniwa ili Mwenyezi Mungu Awapambanue wakweli na wadhaifu, walio imara na waoga.

*Upendo mwanzoni huwa kaidi na katili
ili asiyehusika akimbie.⁸*

⁸ Tafsiri ya ubeti wa Kiajemi

Jaribio liwasibulo manabii na mawalii katika siku za awali na juu ya wao kuwa wapendwa lawadhihirisha kama ndio wadhalilifu, na juu ya kuwa wenye kukubaliwa lawaonyesha kama ndio wenye kukataliwa. Jaribio hilo haliwashukii ili kuwadhalilisha na kuwafedhehesha na kuwaangamiza au kuwafutilia mbali jina lao na alama yao duniani. Kwani, hii haiwezekani kabisa kwamba Mungu Mwenye shani na jalali Awafanyie uadui wale wampendao na kuwaangamiza kwa dhila wapenzi Wake wakweli na waaminifu, bali kwa kweli jaribio lile lishukalo kama simba na mfano wa giza totoro, huteremka ili liwafikishe hao watu wema kwenye mnara mrefu wa kukubaliwa na kuwafundisha elimu za kina sana ya utambuzi wa Mungu. Hii ndiyo suna ya Mungu ambayo tangu zamani Mwenyezi Mungu Amekuwa Anaitumia kwa waja Wake wapenzi. Katika Zaburi, vilio vya unyenyekevu katika hali ya Hadhrat Daud a.s. kujaribiwa vinaidhihirisha suna hii. Na ndani ya Injili, maombolezo ya Hadhrat Masihi a.s. wakati wa majaribio yanathibitisha desturi hii hii ya Mungu. Na ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume s.a.w., maombi ya unyenyekevu ya aliye Fahari ya Mitume s.a.w. yafafanua kanuni hii hii ya asili.⁹ Kama majaribio hayo yasingekuwepo katikati,

⁹ Ndani ya Zaburi, mionganini mwa dua za Hadhrat Daud a.s. alizoomba wakati wa majaribio, mojawapo ndiyo hii: Ee Mungu, Uniokoe, maana maji yamefika mpaka nafsini mwangu. Ninazama

Manabii na Mawalii wasingeweza hata kidogo kuyapata madaraja hayo ya juu waliyopata kwa baraka za majaribio. Majaribio yalipiga muhuri juu ya tabia ya uaminifu wao kamili na dhamira yao ya kudumu na jitihada yao na yakathibitisha kwamba katika wakati wa matetemeko ya majaribio wana

katika matope mengi, pasipowezekana kusimama... Nimechoka kwa kulia kwangu. Macho yangu yamedhoofu... Wanaonichukia bure ni wengi kuliko nywele za kichwa changu. Ee Bwana, Mungu wa majeshi, wanaokungoja Wewe wasiaibishwe kwa ajili yangu. Wanaokutafuta Wewe wasifedheheshwe kwa ajili yangu. Waketio langoni hunisema, na nyimbo za walevi hunidhihaki... Wewe umejua kulaumiwa kwangu, na kuaibika na kufedheheka kwangu. Nikangoja aje wa kunihurumia, wala hakuna. (Tazameni Zaburi: 69). Kadhalika, kadri alivyojinyenyeka Hadhrat Masihi a.s. usiku wa majaribio ni dhahiri kutoka ndani ya Injili. Usiku kucha Hadhrat Masihi a.s. alikesha na kama vile moyo wa mtu uvunjikavyo kutokana na huzuni, hali ya aina hiyo hiyo ilimshinda. Usiku kucha akaomba dua kwa kulia machozi ili kikombe kile cha balaa kilichokuwa kimekadiriwa kimwepuke. Lakini hata juu ya kulia kote huku dua haikukubaliwa, kwa sababu dua ya wakati wa majaribio huwa haikubaliwi. Halafu yapaswa kutazama kwamba Sayyidna Bwana wetu, Fahari ya Mitume na Muhuri wa Manabii, Hadhrat Muhammad Mteule s.a.w. alipataje shida ya aina aina katika hali ya majaribio. Katika dua moja aliomba kwamba: Ee Mola Wangu, mimi nakushtakia udhaifu wangu na ninalalamika juu ya kizingiti chako kuhusiana na unyonge wangu. Udhalili wangu haufichikani machoni mwako. Nitendee vikali kadri upendavyo, mimi niko radhi mpaka Wewe Uridhie. Sina nguvu yoyote pasipo Wewe. Mwandishi.

uimara wa daraja gani la juu sana, na ni waaminifu wa kweli namna gani, na ni wapenzi wa kweli hata kwamba upepo mkali uliwavumia na makiza totoro yalikuja na matetemeko makubwa makubwa yaliwatokea na wakadhalilishwa na wakahesabiwa kuwa miongoni mwa waongo, walaghai na wadhalilifu na wakaachwa peke yao ukiwani kiasi hiki kwamba hata misaada ya Mungu ambayo walikuwa wakiitegemea sana ikajificha kwa muda fulani, na Mwenyezi Mungu ghafla Akaibadili desturi Yake ya kuwatunza kama mtu akasirikavyo sana, na akawaacha hivyo ndani ya shida na taabu kana kwamba wameghadhibikiwa mno, na Akajionyesha Hawajali kana kwamba Hana huruma nao hata kidogo bali Yuawahurumia maadui wao. Na mlolongo wa majaribio yao yakarefuka mno — jaribio moja likimalizika likashuka la pili, na lile la pili likishia likashuka la tatu. Ilmuradi, kama vile mvua inyeshavyo kwa nguvu sana katika usiku wa giza totoro, vivyo hivyo mvua za majaribio zilivyo-wanyeshea, lakini hawakuachana na dhamira zao imara na madhubuti na wala hawakuzembea wala hawakuvunjika moyo; bali kadiri mzigو wa misiba na shida ulivyowaelemea ndivyo hivyo walivyozidi kupiga hatua mbele, na kadiri walivyovunjwa ndivyo walivyoimarika, na kadiri walivyotishwa kwa matatizo ya njia ndivyo hima yao ilivyoendelea kuzidi na ushujaa wao binafsi ukaendelea kutaharuki. Hatimaye wakatoka wakiwa wameipasi mitihani yote hiyo kwa daraja la kwanza na wakafanikiwa

kikamilifu kutohana na baraka za ikhlasi yao timilifu na taji la heshima na utukufu likawekwa juu ya kichwa chao na shutuma zote za wajinga zikatoweka kama povu kana kwamba hazikuwa kitu. Ilmuradi, si kwamba Manabii na Mawalii hawajaribiwi, bali majaribio huwateremkia zaidi sana kuliko wote, na nguvu ya hao tu ya imani huvumilia pia majaribio hayo. Kama watu wa kawaida wasivyoweza kumtambua Mwenyezi Mungu ndivyo wanavyoshindwa pia kuwatambua waja Wake halisi, hususan katika nyakati za majaribio ya hao wapendwa wa Mungu, watu wa kawaida huwa wanadanganyika sana kana kwamba wanaghariki na hawawezi kufanya subira ya kuingojea hatima yao. Watu wa kawaida hawafahamu kwamba ule mmea Aupandao Mungu mwenye jalali na shani kwa mkono Wake huwa Hapogoi matawi yake kwa shabaha ya kuuangamiza, bali hufanya ili mmea huo ulete maua na matunda zaidi na uwe na baraka katika majani na matunda yake. Basi, kwa kifupi ni kwamba kwa ajili ya ulezi wa ndani na ukamilifu wa kiroho wa Manabii na Mawalii ni lazima wapate kujaribiwa. Na majaribio kwa ajili ya watu hawa ni jambo la lazima kana kwamba ndiyo sare ya kiroho ya hao maaskari wa Mungu ambayo watambulikana kwayo. Na yule mtu apataye ufaulu wowote kinyume na suna hii, basi hiyo ndiyo kughilibu wala sio ufaulu. Na pia ikumbukwe kwamba ni bahati mbaya ya hali ya juu na ni mkosi kwamba mtu aiinamie dhana mbaya haraka sana na alichukulie hili kuwa kanuni kwamba

wale wanaodai duniani kwamba wako katika njia ya Mwenyezi Mungu, hao wote ndio walaghai na wadanganifu na wenyewe kutafuta tu maslahi. Kwani, kutokana na itikadi mbovu ya aina hii, mtu taratibu anaanza kuingiwa na shaka juu ya kuwepo kwa uwali na baada ya kuukana uwali basi utazalika wasiwasi kidogo kidogo kuhusu cheo cha unabii, na halafu baada ya kuukana unabii basi dukuduku na shaka kiasi fulani zikizalika katika imani ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na moyo utaanza kudanganyika kwamba pengine habari hii yote ni ya kubuni tu, wala haina msingi na pengine hizi zote ni dhana tu potofu ambazo zimekuwa zikigandama ndani ya mioyo ya watu. Basi, enyi mwapendao ukweli kwa moyo na roho, na mlionaa na njaa na kiu ya ukweli, mfahamu kwa yakini kwa kuondoka penye misukosuko (dunia) na imani salama, kuuyakini uwali na yanayoulazimu ndiyo mionganoni mwa mambo ya lazima. Uwali ni kimbilio la itikadi ya unabii, na unabii ni kimbilio la ikirari ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo mawali kwa ajili ya kuwepo kwa manabii ndio kama nondo, na manabii kwa kuimarishe imani ya uwepo wa Mwenyezi Mungu hufanana na misumari imara.

Basi, yule mtu ambaye hana maarifa ya kumshuhudia walii, macho yake yatashindwa hata kumtambua nabii, na yule asiye na utambuzi kamili wa nabii, ye ye mtu huyo hukosa utambuzi kamili wa Mwenyezi Mungu pia, na lazima siku moja atajikwaa, na atajikwaa vibaya sana, na dalili za kiakili pekee na

elimu za kawaida hazitafaa kitu. Sasa kwa ajili ya faida ya wote tunaona inafaa kuandika pia kuwa kifo cha Bashir Ahmad hakikutokea kwa ghafla, bali Mungu Mwenye shani tukufu, kabla ya kifo chake, Alinipatia utambuzi kikamilifu kwa njia ya funuo zake kwamba huyu mtoto amekwisha maliza kazi yake¹⁰ na sasa atafariki. Bali, zile funuo

¹⁰ Kuna njia mbili adhimu za Mwenyezi Mungu kuteremsha rehema na kutoa baraka za kiroho:

1. Ya kwanza ni kwamba Akiteremsha msiba fulani na huzuni Afungue milango ya msamaha na rehema kwa wafanyao subira kama Mwenyewe Alivyo sema:

وَبَشِّرُ الصَّابِرِينَ إِذَا أَصَابَهُمْ مُّصِيبَةٌ قَاتِلُوا إِنَّمَا اللَّهُ وَإِنَّمَا إِلَيْهِ رَجُونُنَّ^{۱۰}
أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوةٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهَمَّدُونَ^{۱۱}

(Al-Baqarah, 2:156-158)

Yaani kanuni yetu ya asili ndiyo hii kwamba Tulikuwa tunawaletea waaminio misiba ya aina mbali mbali, na rehema zetu huwateremkia wafanyao subira na njia za mafanikio hufunguliwa kwa wale tu wanaofanya subira.

2. Njia ya pili ya kuteremsha rehema ni kutuma mitume na manabii na maimamu na mawalii na makhalifa ili watu waje kwenye njia iliyonyooka kwa kuwafuata na kwa kuongozwa nao, na wakiiga mfano wao wapate kuokoka. Basi, Mwenyezi Mgunu Ametaka kwamba kwa kupitia wazao wangu sehemu zote hizi mbili zipate kudhihirika. Hivyo, kwanza Alimtuma Bashir kwa kuteremsha rehema ya aina ya kwanza ili Akiwaandalia waaminio vifaa vya

وَبَشِّرُ الصَّابِرِينَ

zilizofunuliwa siku aliyozaliwa mtoto huyu aliyefariki nazo ziliashiria kwenye kifo chake na ilionekana kwamba yeye atakuwa ni sababu ya jaribio

Atimiza maana ya Ubashiri Wake. Hivyo, yeye, kwa ajili ya maelfu ya waaminio walioshiriki katika huzuni ya kifo chake kwa ajili ya Mungu tu, akiwa kama mtangulizi wao akawa mwombezi wao kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na ndani kwa ndani akawafikishia baraka nyingi. Na ufunuo wa Mungu ulidhihirisha wazi wazi jambo hili kwamba yule Bashir ambaye amefariki hakuja bila ya faida, bali kifo chake kitakuwa sababu ya uhai kwa watu wote hao ambao kwa ajili ya Mungu walikihuzunikia kifo chake na kuvumilia jaribio hili lililodhihirika kutokana na kifo chake. Ilmuradi, Bashir alizaliwa kama mwombezi kwa ajili ya maelfu ya wenye subira na wakweli. Na kifo cha yule aliyekuja akiwa mtukufu na kuondoka akiwa mtukufu kitakuwa ni kafara ya hao waaminio wote.

Na aina ya pili ya rehema ambayo tumeieleza sasa hivi, kwa kuikamilisha Mwenyezi Mungu Atamtuma Bashir wa pili, kama ilivyotabiriwa kuhusu habari hii kabla ya kifo cha Bashir wa kwanza ndani ya tangazo la tarehe 10 Julai 1888. Na Mwenyezi Mungu Alinidhihirishia kwamba: Utajaliwa Bashir wa pili ambaye jina lake ni Mahmud pia; atakuwa imara katika kutekeleza kazi zake,

يَخْلُقُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ

Mungu Huumba Atakacho. Na Mwenyezi Mungu Amenidhihirishia pia kuwa bishara ya tarehe 20 Februari 1886 kwa hakika ilieleza kuzaliwa kwa wavulana wawili wema, na hadi kwenye ibara hii kwamba ‘Amebarikiwa yule ajaye toka mbinguni’ ilikuwa ni bishara inayomhusu Bashir wa kwanza ambaye akawa kiroho sababu ya rehema kuteremka. Na ibara ya baada yake yamhusu Bashir wa pili. Mwandishi.

kubwa kwa ajli ya viumbe wa Mungu, kama ulivyo ufunuo huu:

إِنَّا آزَسْلَنُهُ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا كَصَيْبٍ مِنَ السَّمَاءِ
فِيهِ ظُلْمٌ وَرَغْدٌ بَرْقٌ كُلُّ شَيْءٍ تَحْتَ قَدَمِيْهِ

Yaani, Sisi Tumemtuma mtoto huyu akiwa mwenye kutoa ushahidi, na mwneye kutoa habari njema na mwenye kuonya. Na huyu anafanana na mvua kubwa ambamo kuna kiza cha namna namna na radi na umeme pia. Vitu vyote hivi viko chini ya miguu yake miwili, yaani, vitakuja kudhihirika baada ya yeze kunyanya miguu yake, na mradi wake ni kifo chake. Hivyo, kiza mradi wake ulikuwa ni kiza cha mitihani na majoribio waliyokabili watu kutokana na kifo chake, na walikumbwa na jaribio kubwa liliokuwa kama kiza na wakawa kama ilivyoelezwa katika aya:

وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَاتِلًا¹¹

Na katika ibara ya ufunuo kama vile baada ya kiza ikatajwa radi na mwanga, yaani kama vile inavyodhihirika katika utaratibu wa maelezo ya ibara hii kwamba baada ya mtoto huyo aliyefariki kuaga dunia kitakuja kiza cha kwanza halafu radi na umeme, ndivyo ilivyoanza kutimia bishara hii kwa utaratibu huu huu; yaani kwanza kwa sababu ya kifo cha Bashir kiza cha jaribio kikatokea na halafu baada yake radi na mwanga vitakuja dhihirika. Na kama vile

¹¹ Na linapowawia giza, husimama. Al-Baqarah, 2:21.

kiza kilikuja dhihirika, vivyo hivyo ifahamike kwa yakini kuwa ile radi na mwanga pia vitakuja dhihirika ambavyo vimeahidiwa. Mwanga ule utakapokuja utayafuta kabisa mawazo yeny kiza toka vifuani na mioyoni, na utazifuta na kuzitokomeza zile shutuma zilizotoka kwenye vinywa vya walioghafilika na wenyе mioyo isiyo na uhai. Ufunuo huu ambao tumeuandika sasa hivi, waliambiwa tangu awali kwa kirefu mamia ya watu. Miongoni mwa waliousikia yumo pia Maulawii Abu Said Muhammad Husain wa Batala na watu wengine wengi waheshimiwa. Sasa kama wanaotuafiki na wanaotupinga wakiyatrafakari madhumuni ya ufunuo huo na kuangalia kwa makini, basi yadhihirisha tu kwamba kuja kwa kiza hiki, tangu mwanzo Mwenyezi Mungu Alikuwa Ameshadhamiria ambayo ilielezwa kwa njia ya ufunuo na ilidhihirishwa kwa uwazi kabisa kwamba kiza na mwanga, vyote viwili, vimo chini ya miguu ya mvulana huyu, yaani baada ya yeze kunyanya miguu — na mradi wake ni kifo chake — havina budi kutokea. Basi, enyi watu ambao mmekwishaliona giza msitaharuki, bali furahini na rukeni kwa furaha, kwani baada ya hapo sasa nuru itakua. Kama vile kifo cha Bashir kilivyotimiza bishara hii, vivyo hivyo kilivyotimiza bishaa ile pia iliyomo ndani ya tangazo la tarehe 20 Februari kwamba baadhi ya watoto watafariki katika umri mdogo.

Mwishoni, ibainike pia hapa kwamba kwa ajili ya kazi zetu twamtegemea kikamilifu kabisa Mola wetu Mkarimu. Hatujali kwamba watu wanaafikiana nasi au wana unafiki, wanayakubali madai yetu au wanayakataa, na wanatusifu au wanatukemea. Bali twashughulikia kazi yetu kwa kujiweka mbali na wote hao huku tukimfahamu asiyekuwa Mungu kama mfu. Ingawa mionganoni mwetu na wanaotokana na kaumu yetu wako baadhi yao ambao wanadharau njia yetu hii, lakini twawaona wana udhuru, na twafahamu kuwa kile tulichodhahirishiwa wao hawaku-dhahirishiwa, na ile kiu tuliyopewa wao hawanayo.

كُلُّ يَعْمَلٍ عَلَىٰ شَكِيرٍ^{١٢}

Hapa naona inafa kuandika hii pia kwamba nimefahamu kutokana na maandishi ya kinasaha ya baadhi ya watu wenye elimu kuwa wao nao hawaupendi mwenendo wangu huu wa kuwadhirishia watu mfululizo wa baraka za kiroho na ishara za kimbunguni unaokamilika kwa njia ya maombi kukubaliwa na ilhaam na kashfi. Mionganoni mwao baadhi yao wanahoji kwamba mambo haya ni ya dhana tu na yenye shaka na matarajio ya madhara yake ni mengi zaidi kuliko faida yake. Hao wanasema pia kwamba kwa hakika mambo haya yanapatikana kwa usawa baina ya wanadamu wote; pengine

¹² Kila mmoja hufanya kwa njia yake. Banii Israaiil, 17:85.

yanazidi kidogo au kupungua kwa baadhi yao; bali baadhi ya watu wanafikiri kuwa ni karibu sawa sawa kwa wote. Pia wanaeleza kuwa mambo haya hayahusikani katu na dini, ucha Mungu na uhusiano na Mungu, bali hizo ni sifa za asili zilizomo nadni ya asili ya mwanadamu, na zinatokea kidogo au zaidi kwa kila mtu akiwa mwaminio au kafiri, mwema au mwovu. Hayo ndiyo mahojiano yao ambayo yaweza kukisiwa kwayo fahamu yao ndogo, fikara zao za kijuujuu na kiwango chao cha elimu. Lakini kutokana na busara sahihi yaonekana pia kwamba busara yao ya kiimani imeliwa kabisa na mdudu wa mghafala na huba ya dunia. Miongoni mwao wapo ambaao hali yao ni kama hali ya ukoma wa mkoma ambaao kwa kukifiki kiwango cha juu unasababisha kukatika viungo, na mikono na miguu huanza kuoza. Halikadhalika viungo vyao vya kiroho — ambavyo mradi wake ni nguvu za kiroho — vimeanza kuoza kutokana na kuipenda dunia kupita kiasi na tabia yao ndiyo tu kukejeli, kudhihaki, kuwa na dhana mbaya na kushuku. Wako huru wasitafakari kwa makini maarifa na kweli za dini. Bali watu hao hawajali kabisa ukweli na maarifa, na wala hawazingatii kwa nini tumekuja duniani, na ni nini ukamilifu wetu asilia, bali usiku na mchana wanahangaikia mzoga wa dunia. Hisia hii haikubakia ndani mwao kwamba wachunguze hali yao namna ilivyoachana na njia za ukweli. Na bahati yao mbaya sana ndiyo kwamba wanaufikiria ugonjwa wao huu wa hatari sana kuwa

siha kamili na ile iliyio siha na afya ya kweli, wanaidunisha na kuhafifisha. Na taadhima ya ubora wa uwalii na ukaribu wa Mungu imeondoka kabisa mioyoni mwao. Na imepaitikana hali kama ya kukata tamaa na fikara kwamba wamenyimwa. Bali kama ikiendelea hali hiyo, kuendelea kwao na imani katika unabii kwaonekana hatarini.

Hii hali mbovu na yenye kutisha niliyoieleza ya baadhi ya wanazuoni, sababu yake siyo kwamba wao kutokana na tajiriba wanafikiri kuwa hizi nuru za kiroho haziwezekani au ni zenye shaka na za kudhania tu, kwani hadi sasa hawajaelekea kujaribu kikamilifu, wala hawajajitafutia fursa ya kueleza maoni yao kwa kuiangalia hiyo kikamilifu na kitimilifu, wala hawajali kupata fursa hiyo. Kwa kuziona tu shutuma zile za kifisadi walizozitoa wapinzani wenyе tabia ya chuki kuhusu bishara zangu mbili,¹³ wakaingiwa na shaka bila ya kufanya utafiti na uchunguzi, na wakaimarisha moyoni itikadi kuhusu nuru za uwalii na za ukaribu na Mungu iliyokaribiana na falsafa kavu na udaharia uliopofuka. Walipaswa kufikiria kwamba wapinzani walitoa uthibitisho gani kusaidia ukadhibishaji wao? Halafu, kama hakuna uthibitisho wowote bali ni porojo tu,

¹³ Shutuma hizo ni hizi kwamba ndani ya tangazo la tarehe 8 Aprili 1886 nilichapisha bishara kwamba mwana mmoja atazaliwa nyumbani kwangu, na ndani ya tangazo hilo niliandika kwa uwazi

basi je, kuathirika moyoni na athari za uzushi wa kipuuzi usio na msingi ni akili au imani thabiti? Na hata kama lingefanyika kwangu kosa la kijtihadi kuhusiana na bishara hii, yaani kwa yakini kabisa

kabisa kwamba pengine yule mwana atazaliwa safari hii au katika himila nyingine ya baada ya hii. Basi, kwa kudhihirisha uchafu wa ndani na ukosefu wa uadilifu wa wapinzai, safari hiyo yaani katika himila ya kwanza, Mwenyezi Mungu Akafanya kuzaliwa mtoto wa kike, na kutokana na himila iliyofuata baada ya hiyo akazaliwa mtoto wa kiume, na bishara ikatokea kuwa ya kweli sawa sawa na muradi wake na ikatimia barabara. Lakini wapinzani, kama ilivyo tabia yao tangu zamani, wakatoa lawama hii kwa kukorofisha kwamba mbona safari ya kwanza mtoto wa kiume hakuzaliwa? Wakajibiwa kuwa katika tangazo hamkuwa na sharti la kuzaliwa safari ya kwanza bali sharti lenyewe lilikuwa la kuzaliwa hadi kwenye himila ya pili, na imetokea sawa nalo, na bishara imetimia barabara. Hivyo kuishutumu bishara kama hii ni aina mojawapo kati ya aina za ukosefu wa imani. Mwadilifu ye yote hawezu kusema hiyo ni shutuma ya haki. Shutuma ya pili ya wapinzani ni hii kwamba mwana ambaye kuhusiana naye bishara ya tarehe 8 Aprili 1886 ilitolewa, alizaliwa na akafa katika umri mdogo. Jibu lake kwa kirefu limeelezwa ndani ya hotuba hii hii, na muhtasari wa jibu ni huu kwamba hadi leo sisi hatujaandika katika tangazo lolote kuwa huyo mtoto ndiye atakayepata umri mrefu wala hatujasema kuwa huyo huyo ndiye Muslih Mau'udi (Mwana wa Ahadi), bali ndani ya tangazo letu la trehe 20 Februari 1886 kulikuwa na bishara hii kuhusiana na baadhi ya wana wangu kwamba watafariki katika umri mdogo. Hivyo yapasa kufikiri kwamba kwa kifo cha mtoto huyu bishara moja imetimia au imebatilika? Bali funuo zote tulizozieneza

kama ingechapwa kwa njia ya tangazo lolote, hata hivyo haingekuwa sababu ya hitilafu machoni mwa yejote mwenye busara, kwani kosa la kijitihadi ni jambo ambalo hata manabii hawakuepukana nalo. Isitoshe, hadi sasa nimeshajaliwa na Mwenyezi Mungu kashfi za kweli na funuo sahihi karibu elfu saba, na bado mfululizo usiokoma wa maajabu ya

baina ya watu, nyingi kati ya hizo zilikuwa zinaashiria kufariki kwa mtoto huyu. Katika ibara hii ya tangazo la tarehe 20 Februari 1886 kwamba: 'Mwana mzuri aliyetakasika anakuja akiwa mgeni wako', neno hili la 'mgeni' kwa hakika ni jina alilopewa mwana huyo huyo. Na hilo laashiria kupata kwake umri mdogo na kufariki mapema, kwani mgeni ndiye yule ambaye hukaa siku chache na kuondoka, na punde si punde anaaga; na yule ambaye huwasindikiza wengine hawezi kuitwa jina mgeni. Na ibara hii ya tangazo hilo kwamba yeje ameepukana kabisa na uchafu (yaani dhambi) pia inatoa dalili ya kufariki kwake katika umri mdogo. Na haifai kudangayika kwa kudhani kwamba ile bishara inayozungumziwa yamhusu Muslih Mau'udi (Mwana Aliyahidiwa), kwa sababu imebainika kwa uwazi kabisa kwa njia ya ufunuo kwamba ibara zote hizo zinamhusu mwana huyo aliyefariki, na bishara inayomhusu Muslih Mau'udi inaanzia kutoka ibara hii: 'Pamoja naye kuna fadhili itakayokuja pamoja na kuja kwake.' Hivyo, Muslih Mau'udi ameitwa jina Fadhili katika ibara ya ufunuo. Na jina lake la pili ni Mahumud na pia jina lake la tatu ni Bashir Thani (wa pili), na katika ufunuo mmoja jina lake liimedhihirishwa kuwa ni Fadhli Umar. Na lazima ujaji wke ungeahirishwa hadi Bashir huyu aliyefariki kuzaliwa na kisha

kiroho kwa siku zijazo unaendelea ambayo yanadumu kuteremka usiku na mchana kama mvua. Hivyo, katka hali hii, mtu mwenye bahati njema ni yule ajisalimishaye kwa Mpango wa Mweneyzi Mungu

kufariki, kwani hekima ya Mungu ilikuwa imeyaweka mambo yote haya chini ya nyayo zake. Na Bashir wa kwanza ambaye amefariki alikuwa ni mtangulizi wa Bashir wa pili, ndiyo sababu wote wawili wakatajwa katika bishara ile ile moja.

Sasa aliye mwadilifu afikirie kwa uadilifu kwamba katika hizo bishara zetu mbili kwa hakika mna kosa gani? Naam, tulidhihirisha kwa njia ya ilhaam sifa bora alizojaliwa mtoto huyo aliyefariki kwamba ye ye kitabia yuko hivi na hivi, na hata sasa twasema hivyo hivyo. Na kupatikana vipawa tofauti vya asili katika watoto bila kujali wapate kufariki utotoni au wabaki hai ni suala ambalo dini zote zinaafikiana; na hakuna ye yeyote mionganoni mwa wanafalasafa na wanazuoni awezaye kulikataa hilo. Basi, kwa mwenye busara kuna sababu gani ya kupotoka? Naam, basi, watu wajinga na wapumbavu wameendelea siku zote kupotoka. Wana wa Israeli wakapotoka kwa bishara ya Hadhrat Musa a.s. kwamba mtu huyu alikuwa akisema kwamba adhabu itamteremkia Firauni, lakini adhabu haiku- mteremkia hata kidogo bali adhabu ile imetukumba sisi, kwani hapo kabla tulikuwa tukifanyishwa shokoa kwa nusu siku tu na sasa limetoka agizo la kufanyishwa shokoa kwa siku nzima. Wokovu ulioje huu tulipata!! Kwa hakika kufanyishwa huku shokoa maradufu kuliwateremkia Wayahudi hapo mwanzoni kama jaribio, lakini hatimaye hilaki kwa Firauni ilikuwa imekadiriwa, lakini hao wapumbavu na wenye papara wasipoona kutimia habari hii haraka sana wakaanza kumkadhibisha Hadhrat Musa a.s. na wakaingwa na

kwa ikhlasi na usafi wa moyo na kujinufaisha nafsi yake na baraka za kimbunguni. Na mwenye bahati mbaya sana ni yule mtu ambaye asipojali kujipatia hizo nuru na baraka awe na mwenendo wa kutoa shutuma zisizo na msingi na kudhihirisha rai ya kijinga. Mimi kwa ajili ya Mungu tu nawatanabahisha watu hao kwamba kwa kuingiza miyoni mawazo ya aina hii wameenda mbali sana na ukweli na kuuona ukweli. Kama kauli yao hii ni ya kweli kwamba funuo na kashfi si kitu chenye thamani kinachoweza

dhana mbaya na wakasema ewe Musa na Haruna! Mungu Akutendeeni kile mlichotutendea.

Kisha inafaa kutazama ujinga na papara ya Yuda Iskariote kwamba alipotoka sana katika kuzielewa bishara za Hadhrat Masihi a.s. na akadhani kwamba mtu huyu alikuwa anadai kuwa atakuwa Mfalme na kutupatia sisi vyeo vikubwa vikubwa, lakini habari hizo zote zimetokea kuwa ya uongo na hakuna bishara yake yoyote ile iliyotokea kuwa ya kweli, bali sisi tunakufa katika hali ya ufukara na njaa; afadhali kuungana na maadui zake ili tujaze tumbo. Hivyo ujahili wake ukawa sababu ya kuhiliki kwake. Bishara za Hadhrat Masihi a.s. zilitimia katika nyakati zake. Basi, ukadhibishaji wa wakadhibishaji hao wajinga ukawaleta manabii hasara gani ambayo tuiogope hata sasa na kutohana na hofu hiyo kazi tukufu ya Mwenyezi Mungu ifungwe! Yafaa kuzingatia barabara kuwa wale watu ambao wakijiita Waislamu na kutoa shahada wanajikusanyia haraka sana wasiwasi mwingi miyoni mwao, hao hatimaye watafedheheka na kudhalilika kama walivyofedheheka na kudhalilika Wayahudi wabovu na wapotovu na Yuda iskariote. Basi mtafakari, enyi wenye busara.

Mwandishi.

kupambanua wazi wazi baina ya watu makhsus na wa kawaida, au kafiri na mwaminio, basi hili litakuwa jambo la kuwavunja sana moyo Masaliki (walioko njiani katika safari ya kiroho ya kuungana na Mungu). Mimi nawahakikishia kwamba hii tu ndiyo sifa ya kiroho na ya daraja la juu ya Islam kwamba waifuatao kwa ukweli wa moyo wanajaaliwa maongezi makhsus na Mungu, na nuru za kukubalika kwao huwa zinazalika ndani yao ambazo mwingine hawezи kushiriki nao katika hizo. Huu ni ukweli hasa ambaao umeshawabainikia watu wema wasiohesabika kwa tajiriba zao wenyewe. Wafikiao madaraj haya ya juu ndio wale ambaao wanamfuata Mtume wa Mungu s.a.w. barabara, kwelikweli, na wakijivulia dhati ya kinafsi hujivalia dhati ya Kiungu, yaani kwa kuyaua matamanio ya nafsi wanajipatia maisha mapya ndani mwao ya kumtii Mungu katika mambo yote. Waislamu wenyе hali pungufu hawalingani nao sembuse kafiri na fasik. Ukamilifu wao huu huwafungukia watafutao haki kwa kukaa pamoja nao. Kwa sababu hiyo, ili kutimiza hoja, niliwatumia matangazo na kuwaandikia barua viongozi wa madhehebu mbali mbali ili walipime dai langu hili. Kama wangkuwa wanatafuta ukweli, wangkuja kwa moyo safi. Basi, hakuja hata mmoja mionganoni mwao kwa moyo safi, bali wakati bishara yoyote ilipokuwa ikitimia, walikuwa wakijaribu kuihafifisha. Sasa kama wanazuoni wetu wanasisita kuukubali na kuuamini uhakika huu, kuna haja gani ya kuwaita

wengine. Kwanza hao marafiki zetu ambao mionganoni mwao mna wataalamu na wanazuoni, wafanye majaribio na wakae pamoja nami kwa ikhlasi na subira kwa muda fulani, ili wapate kujua uhakika ulivyo, halafu kama dai langu hili lionekane si kweli, basi mimi nitatubu kwa mikono yao, waila natumai kwamba Mwenyezi Mungu Atawafunulia mioyo yao njia ya kutubu na kurejea. Na kama baada ya kuenezwa maandishi yangu haya wayapime madai yangu na kuhakikisha ukweli wa rai yao, hapo maandishi yao ya kinasaha yatakuwa na maana; hadi wakati huu hayo hayana maana hata kidogo. Bali hali yao ya kutokuwa na busara ya kiroho inatia huruma. Mimi nafahamu sana kwamba mawazo yenyenuguu ya siku hizi ya kuitegemea akili yameishinda kiasi fulani mioyo ya wanazuoni wetu pia, maana wanakazania mawazo hayo kupita kiasi na wanayafikiria kwamba yanatosheleza kukamilisha dini na imani, na wanazihakirisha baraka za kiroho kwa njia zisizojuzu na zinazochukiza. Nafikiri hawazihakirishi kwa kujikalifisha, bali hiyo imeimarika katika mioyo yao, na udhaifu wao wa kiasili umejitoa kwa tetemeko hili, kwani ndani mwao mna mng'ao kidogo sana wa nuru ya ukweli na mmejaa maneno mengi yasiyo na kiini. Na huiona rai yao kuwa sahihi kabisa na kukazania sana kuishindania hata kwamba kama ingewezeekana wangewavuta kwenye kiza hicho hata wenye kupata nuru pia. Bila shaka hao wanazuoni wanafikiria

ushindi wa kidhahiri wa Islam lakini hawana habari ya mambo yale ambamo ushindi wa kweli wa Islam umo.

Ushindi wa kweli wa Islam umo katika sisi kujisalimisha kikamilifu kwa Mwenyezi Mungu — kama ilivyo maana ya neno la Islam — na kujitenga kabisa na nafsi zetu na maono yake, na lisibaki njiani mwetu sanamu lolote la tamaa na dhamira na kuabudu viumbe, na tujitokomeze kikamilifu ndani ya radhi za Mungu. Na baada ya kujifia huku tuupate uzima ule ambao utupatie busara yetu hali nyingine na kuyajaalia maarifa yetu nuru mpya na kuyatilia mapenzi yetu uharara mpya na tuwe watu wapya, na yule Mungu wetu wa zamani Awe Mungu Mpya kwa ajili yetu. Huu ndio ushindi wa kweli ambao tawi mojawapo mionganoni mwa matawi yake kadha ni maongezi pia na Mungu. Wasipopata Waislamu huu ushindi katika zama hizi, basi ushindi mtupu wa kiakili hauwezi kuwafikisha popote. Mimi nina yakini kwamba siku za ushindi huu zipo karibu, Mwenyezi Mungu Mwenyewe Atariumba nuru hii na Atakuwa mwokozi kwa waja Wake dhaifu.

KUFIKISHA UJUMBE

Hapa nawafikishia ujumbe mwingine watu wote kwa ujumla na hasa ndugu zangu Waislamu kwamba mimi nimeamriwa kuwa wanaotafuta ukweli wafanye Baiat yangu kwa kupata ujuzi wa imani ya kweli na utakaso

wa kweli wa imani na njia ya upendo wa Mola, na kwa kutengana na maisha machafu na maisha ya uzembe na usaliti. Basi wale wanaoona nafsini mwao uwezo huo kadiri fulani, wanalazimika wanijie, kwani mimi nitakuwa mwenye kuwaliwaza na nitajitahidi kuwapunguzia mzigo wao, na Mwenyezi Mungu Atawajalia baraka kwa dua yangu na mwelekeo wangu ikiwa watakuwa tayari kufuata masharti ya Mungu kwa moyo wote. Hili ni agizo la Mungu ambalo leo nimeshafikisha tayari. Kuhusu habari hii ufunuo wa Kiarabu ndio huu:

إِذَا عَرَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَاصْبِنْ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا
الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ¹⁴

Salamu iwe juu ya afuataye mwongozo.

Mfikishaji, Mnyenyeketu,
Mirza Ghulam Ahmad Mungu Amsamehe
1 Desemba, 1888.

¹⁴ Ufungapo nia, basi Mtegemee Mweyenzi Mungu na ukaunde jahazi mbele ya macho yetu na sawa na ufunuo wetu. Wanaofungamana nawe kwa hakika wanafungamana na Mweyezi Mugnu. Mkono wa Mungu upo juu ya mikono yao.

TANGAZO — la — CHANIKIWITI

Sabz Ishtihaar **The Green Announcement** (*Swahili Translation*)

This book was written by Hazrat Mirza Ghulam Ahmad of Qadian^{as}, the Promised Messiah and Mahdi, Founder of the Ahmadiyya Muslim Community, to remove the doubts and misgivings that had arisen out of the death of his son who has come to be known as Bashir the First. Bashir was born on 7th August 1887 and died on 4th November 1888.

Previously the Promised Messiah^{as} had announced, on the basis of Divine revelations, that Allah had promised to grant him a son who would possess extraordinary qualities, would have a long life, and would be Musleh Mau'ud (the Promised Reformer).

Thus when Bashir the First died after sixteen months, the opponents pounced at the opportunity and began denouncing the Promised Messiah^{as} even more vehemently. In this announcement, the Promised Messiah^{as} made it clear that he had never claimed that this particular boy would be the Promised Reformer. He also forcefully reiterated that the promised child would be born within the nine year period (1886-1895) specified in the prophecy.

Towards the end of the book, the Promised Messiah^{as} also announces that through revelation from Allah, the Almighty, he has been commanded to take the oath of allegiance (Bai'at) so that those who seek truth and desire to find Allah's love may do so through his fervent prayer. Thereby laying the foundation of the Ahmadiyya Muslim Jamā'at.

